Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Ujitokezaji wa Hejemonia Katika Asasi Za Kijamii: Mfano wa *Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti* na *Majilio ya Mkombozi.*

**Harrison Onyango Ogutu[1]; Dr. Sheila Wandera[2]; Prof. Wendo Nabea[3]**
**[1.2.3] Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.**

**Main Author Email: harrynamasumbi@gmail.com**

## IKISIRI

Watu wenye uwezo na mamlaka wanatumia madaraka yao kuwatawala wengine kwa vishawishi anuwai. Asasi za kijamii kama vile ndoa, shule, vyuo, utamaduni na malezi zinaendelea kushuhudia utawala wa wenye uwezo juu ya wasio na uwezo. Licha ya ubayana wa hali hii katika jamii, watafiti na wahakiki wa tanzu za fasihi andishi hususan riwaya hawajaonyesha namna hejemonia inajitokeza katika asasi za kijamii. Ingawa wahakiki wengi wa riwaya wameweza kuangazia masuala ya kila nui kuhusu asasi za kijamii, suala la hejemonia katika taasisi hizo lilihitaji kumulikwa. Hivyo, utafiti huu ulidhamiria kuchunguza ujitokezaji wa hejemonia katika safu ya hejemonia ya jamii kwa mujibu wa riwaya za *Msimu wa Vipepeo, Dharau ya Ini, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Mkombozi.* Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya hejemonia ilioasisiwa na Antonio Gramsci katika makala aliyoyaandika akiwa gerezani kati ya mwaka wa 1923 na 1936. Nadharia hii inaelezea udumishaji wa uwezo na mamlaka ya tabaka moja kuu juu ya tabaka dogo kwa kutumia mikakati anuwai. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ambako utaratibu wa upekuzi wa yaliyomo ulitumika kukusanya data huku mbinu ya kithamano ikitumika kuchanganua data hiyo. Matokeo ya utafiti huu yatawafaa wahakiki na watafiti wa lugha na fasihi huku yakiweka wazi uwepo wa hejemonia katika asasi za jamii.

**Maneno Muhimu:** Hejemoni, Hejemonia, Safu ya hejemonia, asasi za kijamii.

**How to cite this article in APA.**
Ogutu, H. O., Wandera, S. &. Nabea, W. (2020). Ujitokezaji Wa Hejemonia Katika Asasi Za Kijamii: Mfano wa *Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti* na *Majilio ya Mkombozi. Editon Cons. J. Kiswahili,* 2(1), 76-88. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
------------------------------------------------------------------***------------------------------------------------------------------



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

## Utangulizi

Baadhi ya watu katika jamii wanawatawala wanajamii wenzao kwa kuwapumbaza na kuwafanya waridhie na kuidhinisha mawazo, imani na mtazamo fulani wa maisha. Watawaliwa wanakubali mamlaka juu yao kwa hiari kutokana na mwafaka unaowekwa baina yao na watawala. Wamitila (2003) anaeleza dhana ya hejemonia kuwa hali ya kudumisha uwezo au mamlaka juu ya wengine bila ya kutumia nguvu. Katika asasi za kijamii, viongozi wengi wanaonekana wakidumisha utawala wao kwa vishawishi anuwai. Hali hii ya kuwashawishi watu kufanya utakalo kwa namna ya kuvutia, kupendeza na iliyo muhali kupingika ndio Nella (2017) ameiita hejemonia ya kijamii. Watawaliwa wenyewe wanakubali kutawaliwa na hejemoni hususan kwa kukubali vishawishi vya namna kwa namna.

Hejemonia inadhihirika katika kila sekta kama wanavyokiri Artz na Murphy (2000). Wanasema kuwa jamii imesheheni hejemonia; hejemonia katika mashirika, hejemonia katika vyombo vya habari, hejemonia ya mwajiri juu ya mwajiriwa, hejemonia ya mwalimu juu ya mwanafunzi na kadhalika. Kwa misingi hii, mtafiti alichunguza ujitokezaji wa hejemonia katika asasi mbalimbali za kijamii. Asasi za kijamii kama vile familia, ndoa, dini, utamaduni na taasisi za elimu zinaonyesha hejemonia inayokuzwa na kudumishwa na usimamizi wa asasi zenyewe. Hivyo, mtafiti alichunguza usawiri na udhihirisho wa hejemonia katika asasi hizi za kijami mintarafu riwaya za *Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti* na *Majilio ya Mkombozi.*

### Misingi ya nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya hejemonia ilioasisiwa na Antonio Gramsci (1891-1937) katika daftari alizoziandika baina ya 1923-1936 akiwa gerezani. Alidai kuwa hejemonia ni hali ambapo mitazamo, desturi, thamani, itikadi na imani za watu katika jamii hutumiwa na viongozi kwa werevu kuwatawala wengine, Gramsci Antonio (1995). Watu wenye mamlaka na uwezo wanawashawishi walio chini yao kukubali mitazamo, mawazo na imani yao kama hali ya kawaida. Mihimili ifuatayo ilikuwa muhimu kwa uchanganuzi wa data ya utafiti.

Kwanza, hejemonia inategemea mwafaka uliopo kati ya watawala na watawaliwa. Tabaka tawaliwa lazima lipokee faida fulani au linufaike kwa namna fulani kutokana na mwafaka uliowekwa. Mhimili huu ulisaidia kuchunguza namna hejemonia inavyodhihirika katika jamii kutokana ushirikiano, masikilizano na maafikiano kati ya watawala na watawaliwa.

Nguzo nyingine muhimu katika hejemonia ni asasi za kijamii kama vile vyama vya maslahi ya wafanyakazi, dini, taasisi za elimu na familia. Katika uongozi wa kihejemonia asasi hizi zinahitajika kuwapumbaza raia, kuwatosheleza na kuwapa hisia za udhibiti wa mambo yao, Nella (2017). Mhimili huu ulikuwa msingi madhubuti kwa utafiti huu kwani ulisaidia kuonyesha udhihirisho wa hejemonia katika asasi za kijamii kama vile dini, familia na taasisi za elimu.

Pia uongozi wa kihejemonia unaendelezwa kupitia utamaduni wa jamii husika. Hejemonia inawasilishwa kama imani na itikadi ambayo lazima watu waizingatie na kutumia katika jamii. Mathalani, kupitia utamaduni-pendwa, watu wanafunzwa mambo ambayo wanafaa kuyahitaji na kutamani na kisha hatimaye utawala unawasilisha mahitaji hayo kwa raia. Utamaduni unadhihirishwa kupitia makubaliano na kushurutishwa. Makubaliano ni njia ambayo kwayo watu wanashirikishwa katika utawala ama moja kwa moja au kwa njia fiche. Strinati (1995), anadai kuwa watu wanaweza kukubali hali iliyopo kwa sababu wameshurutishwa kufanya hivyo kwa kutumia muda wao


© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

mwingi kujichumia au kwa sababu hawawezi kung'amua njia nyingine yoyote mbadala ya kuunganisha jamii. Nguzo hii ilikuwa muhimu kwa utafiti kwani ilisaidia kudhihirisha namna hejemonia inavyojitokeza kupitia utamaduni wa jamii.

Hatimaye nguzo nyingine ni mchango wa wasomi na wataalamu katika uongozi wa kihejemonia. Wasomi na wataalamu wanaendeleza mawazo na itikadi za kikundi tawala kupitia uvumbuzi na usambazaji wa mawazo, imani na itikadi, Meysam (2014). Wasomi wanashiriki katika shughuli za kijamii kupitia usimamizi wa mashirika. Mintarafu nadharia hii, wanahabari, viongozi wa dini na wasimamizi wa taasisi za elimu wanaamini kuwa wao ndiwo wasomi na wataalamu bora. Hivyo, makanisa na mashirika ya kijamii ni kama uwanja wa wasomi ambapo ama wanapinga hejemonia au wanaunga mkono hejemonia. Mhimili huu ulisaidia kuweka bayana namna ambavyo baadhi wasomi na wataalamu katika asasi za kijamii kama vile dini na taasisi za elimu ama wanaendeleza hejemonia au wanatumiwa na mahejemoni kudumisha hejemonia.

**Hejemonia katika asasi za kijamii**

Safu ya hejemonia ya kijamii imejitokeza bayana kupitia asasi za kijamii kama vile elimu, ndoa, utamaduni, dini na malezi ya watoto katika familia. Katika asasi hizi, imedhidhirika kwamba watu wenye uwezo na mamlaka kama vile viongozi wa dini, wazazi na wanaume katika familia na ndoa wanaonyesha sifa za mahejemoni katika usimamizi wao. Wasimamizi hawa wanawataka walio chini yao ama kwa shuruti au kwa hiari wakubaliane nao ilmradi waendelee kuwatawala. Hali hii inadhihirika katika asasi anuwai za kijamii ifuatavyo.

**Taasisi za Elimu**

Taasisi za elimu kama vile shule na vyuo zinadhihirisha uwepo wa hejemonia katika jamii kupitia usimamizi wa asasi hizo. Suala la elimu na hejemonia limezungumziwa katika *Msururu wa Usaliti.* Elimu ya shule ya msingi inaonewa fahari na mahejemoni katika jamii. Mabepari na mamwinyi katika jamii wanawashawishi na kuwaaminisha raia kwamba elimu ya shule ya msingi inawatosha. Elimu ya shule ya msingi inapigiwa upato na viongozi wa jamii huku elimu ya vyuo vikuu ikidhalilishwa na kuonekana kutokuwa na umuhimu wowote. Mathalani, viongozi wa jamii wanapuuza maendeleo ya Chuo Kikuu cha Kitaifa (CHUKI) kwa misingi kuwa kuboresha chuo kikuu hakuna manufaa yoyote kwa utawala. Kwa hivyo, ili kudumisha na kuendeleza utawala wao juu ya watawaliwa, viongozi wa jamii wanaunga mkono elimu ya shule za msingi kwa madai kuwa inahusu watu wengi wanaowaunga mkono. Watawaliwa wanashawishika kupiga jeki utawala wa kihejemonia kwa kupumbazwa kuwa elimu ya juu haina manufaa yoyote kwao. Hii ndio sababu uongozi wa kihejemonia unanawiri kutokana na idadi kubwa ya raia wasio na elimu ya juu kuutetea na kuupigia debe.

Shule kama vile *Magna Star Academy* katika *Dharau ya Ini* inadhihirisha uwepo wa hejemonia katika jamii. Shule spesheli za watoto wa mamwinyi wanaotawala zinaendeleza hejemonia. Kwa mfano Master John, mtoto wa Munene ambaye ni hejemoni mkubwa anasomea katika shule hii. Watoto wanaosomea katika shule hizi ni wale wanaotoka katika familia za mabepari na mabwanyenye wanaokuza na kuendeleza hejemonia katika jamii. Mahejemoni wanakuwa na shule zao maalum ambazo kulingana nao zinafaa kuwapa watoto wao elimu bora na ya kiwango cha juu kuliko ile inayopatikana katika shule za kawaida. Mabwanyenye wanafanya hivi ili kuwatawala wengine kupitia nyenzo ya elimu. La kusikitisha ni kwamba watoto wa mabepari na mabwanyenye wanaosomea katika shule maalum wanatumia dawa za kulevya kando na kujihusisha katika tabia zingine zinazoonyesha upotovu wa maadili (uk 15



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

na 97). Lakini walimu wanaojaribu kupinga hejemonia kwa kuwaadhibu watoto wa mabwanyenye wanaishia kufutwa kazi kama inavyomfanyikia Katumbi.

Safu ya hejemonia ya kijamii pia inadhihirika kupitia muundo wa usimamizi wa vyuo vikuu. Kwa mujibu wa Profesa Mbogo katika *Dharau ya Ini* uongozi wa vyuo vikuu ni wa kibepari na kimwinyi. Anasema:

> "Ni kama muundo wa Chuo Kikuu. Chuo Kikuu ni asasi inayoishi katika jamii ya kibepari lakini muundo wake ni wa kimwinyi…Angalia wakuu wa idara, vitivo na vyuo vyenyewe…Wanafanana na mamwinyi, yaani *mafeudal lords*, waliokaa kungojea wakulima kuwaletea vipeto vya mazao. Walio chini yao wote ni kama mafalahi, masefule na wajakazi! Wasomi wenyewe wanashindwa kuutangua muundo uliopitwa na wakati. Wasomi hawaendi na wakati! Wakati wa wasomi umekwama. Hauendi!" (uk 248).

Wasimamizi wa vyuo vikuu wanafananishwa na mamwinyi wanaowagandamiza wafanyakazi wa viwango vya chini. Wasimamizi hawa hawataki mabadiliko yoyote katika muundo na mfumo wa usimamizi wa vyuo. Katika asasi ya elimu, hejemonia inakuzwa na kudumishwa na wasomi na wataalamu kwa maridhiano na wafanyakazi wa ngazi za chini. Wasomi na wataalamu katika asasi za elimu wanafananishwa na mabwanyenye wanaozembea huku wakingojea kazi kufanywa na wafanyakazi wa viwango vya chini. Tabia hii ya kimwinyi miongoni mwa wasomi na wataalamu ndio inayodumaza maendeleo katika sekta ya elimu na jamii kwa jumla. Wasomi na wataalamu wanaoshikilia ukale wa mambo ni kama vibaraka wa mabepari wanaomiliki mali na kutumia mali hiyo kukuza utawala wao. Uhafidhina wa wasomi na wataalamu unachochea kukua na kuendelea kwa hejemonia katika taasisi za masomo hususan vyuo vikuu. Si ajabu basi kupata kwamba viongozi wakisiasa kwa kutambua udhaifu huu miongoni mwa wasomi, wanatumia wasomi na wataalamu kusambaza sera zao za kihejemonia katika jamii. Hali hii ni bayana kupitia kufukuzwa kutoka chuoni kwa vijana wanamapinduzi kama vile Kage na wenzake katika *Msururu wa Usaliti* na pia baadhi ya vijana wanaoandamana kupinga Waziri Mkurutu na utawala wake katika *Msimu wa Vipepeo*. Wasimamizi wa vyuo vikuu wanashirikiana na mabwanyenye serikalini kukatiza elimu ya vijana wanaokosoa na kupinga hejemonia inayokuzwa na kudumishwa.

**Familia na Malezi**

Safu ya hejemonia ya kijamii pia inadhihirika kupitia malezi ya watoto katika familia. Katika *Msururu wa Usaliti* babake na mamake kijana Kage (Mheshimiwa Mbogo na Makena mtawalia) wanamtaka binti yao asomee taaluma ya utabibu kinyume na anavyotaka binti yao; kusomea taaluma ya Sayansi ya Mazingira. Baada ya Kage kuhitimu elimu ya chuo kikuu na kupata shahada ya Sayansi ya Mazingira kutoka Chuo Kikuu cha Thames – Uingereza, babake mzazi anafanya jitihada za kutaka kumtawala bintiye tena. Mheshimiwa Mbogo anatumia vishawishi vya kila namna kumtawala bintiye kimawazo. Kwanza, anataka kumtafutia kazi ama serikalini au katika sekta ya kibinafsi. Anamwambia bintiye hivi; "Nataka kutumia uhusiano wangu na watu wazito kukupatia 'kazi ya maana'. Nataka tu uniambie kazi unayoitaka chaguo ni lako," (uk 29). Malezi ya mzazi kumpa mtoto zawadi ili aendelee kunyenyekea na kuunga mkono yote anayoyafanya hata kama ni maovu ni juhudi za kukuza na kudumisha hejemonia katika familia. Wazazi wanatumia uwezo na mamlaka yao kuamua mkondo wa maisha wa watoto wao na kwa njia hiyo wanaishia kuwatawala.

Hejemonia inajitokeza katika hali ambapo wazazi wanawabembeleza watoto wao kusomea taaluma



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

ambazo wazazi hao wanazionea fahari mintarafu *Msururu wa Usaliti*. Wanawaonyesha na kusifia taaluma hizo ili kuwasadikisha watoto kuwa maoni yao kuhusu kozi na taaluma hizo ndio bora zaidi. Baadhi ya watoto kwa kuhofia uwezekano wa kuadhibiwa na wazazi wao wanaridhia matamanio na matakwa ya wazazi. Watoto katika familia wanashawishika kusikia ushauri wa wakuu wao kwa kuhofia kuvunjika guu iwapo wataenda kinyume na ushauri wanaopewa na wazazi. Wazazi wanawanyima watoto wao uhuru wa kujichagulia taaluma wanazotaka kusomea. Ingawaje watoto wana uwezo wa kufanya uamuzi kuhusu mustabali wa maisha yao, wazazi wanawatia uwoga na kuwanyima fursa hiyo. Inadhihirika kwamba baadhi ya wazazi katika jamii wanatumia wajibu wao wa malezi ya watoto kama fursa ya kukuza hejemonia katika familia. Wazazi kama hawa wanadhihirisha sifa za mahejemoni katika familia.

Malezi katika familia kama kipengee cha safu ya hejemonia ya kijamii ni suala linalodokezwa na mwandishi wa *Msimu wa Vipepeo*. Hejemonia katika familia na malezi inajitokeza kupitia namna Mkurutu na Julia wanamlea Ndumi. Kwanza, Julia anajaribu awezavyo kumwaminisha Ndumi kuwa Mkurutu ndiye babake lakini Ndumi anakataa kwa kusisitiza kuwa anajua fika kuwa babake ni Kanda. Julia, anambembeleza na kumtaka Ndumi atupe katika kaburi la sahau maisha ya umaskini walioishi awali wakiwa na babake – Kanda. Maisha ambayo yalidhihirisha uchochole kwa watoto kucheza kibafute, wengine wakikimbiza kibaramwezi na wavulana wakikimbizana na kucheza kandanda kwa mipira midogo ya matambara huku wakitifua vumbi.

Pili, waziri Mkurutu anadhihirisha sifa za hejemoni katika familia kwa namna anavyomlea Ndumi (binti yake wa kambo). Anatoa onyo kwamba kamwe hatairuhusu familia yake kurudi misri walikotoka (kwenye maisha ya dhiki na ufukara mtupu). Yuko tayari kumtosa yeyote gerezani hata Kanda, babake Ndumi; akaozee huko kama mizizi ya misubili. Vitisho vya namna hii ni njia mwafaka inayotumiwa na watu wenye uwezo kuwatia hofu na uwoga watu wasio na uwezo ili wakubaliane na utawala wao. Mkurutu anapata wakati wa kuandamana na Ndumi kwenda kununua vitabu, kwenye sherehe za kuzaliwa za marafiki na hata kufuatilia maendeleo yake ya kujifunza kucheza piano. Zaidi, waziri anamnunulia Ndumi simu ya mkononi ya kipekee yenye kamera na uwezo wa kuhifadhi picha za video.

Kwa mujibu wa *Msimu wa Vipepeo,* katika baadhi ya familia wazazi wanakuwa mahejemoni wanaotumia uwezo wao kama walezi kuwatawala watoto kwa vishawishi vya kila nui. Wazazi hawa wanafanya hivyo kwa kuwaaminisha watoto wao kwamba yote wanayoyasema na kuyafanya ni kwa manufaa ya watoto. Wazazi wanatarajia watoto kuzingatia manufaa na faida wanazopata ili wasikilizane na kukubaliana nao kwa yote wanayoyasema na kutenda. Msimamo huu wa wazazi unachangia ukuaji na udumishwaji wa hejemonia ya kijamii kupitia malezi ya watoto katika familia. Kwa hivyo, wazazi wanaishia kuwa mahejemoni katika familia kwa kutumia vishawishi mbalimbali kutafuta ridhaa ya watoto. Mintarafu utafiti huu, wazazi wanakuwa mahejemoni katika familia kwa namna wanavyowalea watoto wao. Aghalabu wazazi wanawataka watoto wao kuwaiga kama kielelezo katika maisha. Si ajabu kupata kwamba pale ambapo watoto wanakosa kukubaliana na wazazi wao, nguvu na vitisho vinatumika kuwatia hofu watoto ili wakubali, waridhie na kuidhinisha hejemonia inayokuzwa na wazazi hao.

**Ndoa**

Hejemonia ya kijamii pia imebainika wazi katika asasi ya ndoa. Ndoa ni taasisi ya kimsingi katika ujenzi wa familia na jamii kwa jumla. Ndoa nyingi zinashuhudia hejemonia inayokuzwa na mume au mke. Mathalani, katika *Dharau*



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

*ya Ini* Munene katika ndoa zake za kwanza mbili anadhihirisha mamlaka na uwezo wa hejemoni kama mume na kiongozi wa boma. Anawatawala wake zake na kuwalaumu kwa kutomzalia watoto wa kiume. Kama mume katika ndoa, Munene anaonyesha mamlaka na uwezo juu wake zake. Ndoa ya Munene na mke wake wa kwanza Kasina inaanza kwa mapenzi ya kupigiwa mfano. Munene na ubabedume wake na jinamizi la kumzaa mtoto mvulana akaangusha ini mchangani. Msingi wa ndoa imara katika jamii hii ni mke kumzaa mtoto mvulana. Tunaona kuwa, Deborah anapomzalia Munene mtoto mvulana ndoa inadumishwa licha ya kwamba Munene ni katili, hamtaliki Deborah. Kila mara anapokumbuka kuwa amemzalia mtoto wa kiume, anajizuia kumpiga. Mwandishi akimrejelea Munene anasema: "Alishindwa kumkemea Deborah. Labda… alikuwa ule mbuyu usemwao na watu kwao kijijini. Kila shetani ana mbuyu wake," (uk 26). Utamaduni unaomthamini mtoto wa kiume unamfanya Munene asimkemee mkewe kwa sababu ya kumzalia mtoto wa kiume. Mkewe naye kwa werevu anatumia fursa hiyo kumtawala Munene. Hejemonia katika ndoa haiwezi kunawiri pasi ya mazingira ya ndoa kuiruhusu. Lazima mmoja kati ya wanandoa awe ameruhusu hali hiyo kuwepo. Katika nyingi ya ndoa zinazoshuhudia hejemonia, mume ama mke huwa ameridhia kuwepo kwa hali hii katika ndoa yake.

Wanawake wanaogundua udhaifu wa waume zao wanatumia mazingazi ya ndoa kupambana na hejemonia inayokuzwa na wanaume. Kwa hekima na werevu, mwanamke katika ndoa anageuzwa na tamaa ya mumewe kuwa hejemoni mwenye mamlaka makubwa juu ya mumewe. Hii ndio sababu Deborah anapozaa mtoto wa kiume anatumia mizungu ya ndoa kukuza hejemonia juu ya mumewe (Munene) katika *Dhararau ya Ini*. Mtoto wao (*master* John), anapokuwa mkubwa na kutambua namna jamii inavyomthamini mtoto wa kiume na ilhali ni yeye wa pekee katika familia hii, pia anaishia kutumia mazingazi ya ndoa na kuibuka hejemoni anayewatawala wazazi wake. Anajichagulia shule anayotaka na mambo mengine mengi kwa kudekezwa na babake mzazi ambaye kimsingi anafaa kumtia adabu mwanawe. Kwa mjibu wa mtafiti, hejemonia katika ndoa inakuzwa kutokana na imani za kitamaduni; utamaduni unaomwaminisha mwanajamii kuwa ndoa isiyokuwa na mtoto wa kiume ni ndoa dhaifu. Hivyo wanajamii wanasadikishwa kuwa ili kudumisha ndoa, lazima mke aweze kumzaa mtoto mvulana. Wanawake wengi katika jamii wanawezesha kuwepo kwa hejemonia wanapokubaliana na mawazo kama hayo ambayo aghalabu yanakumbatiwa sana na wanaume wanaokuza hejemonia.

Suala la hejemonia katika ndoa linaendelea kujitokeza kupitia ndoa ya Wanza na King'o katika *Dharau ya Ini*. Wanza ni mfano mzuri wa wanawake ambao wanaenda kinyume na hejemonia ya kijamii. Wanza anaonekana kupinga utamaduni huu anapokabiliana na mumewe kwa kumpiga akimtaka awajibike nyumbani. Wanajamii kwa kutotarajia kitendo cha namna hii kinachoenda kinyume na utamaduni wa jamii yao katika ndoa, wanamsuta na kumbeza King'o hivi; "Hiki ni nini alichooa huyu? Kaoa au kaolewa jamani?" (uk 41). Wanajamii wanashangazwa na hali ambapo mwanamume anaweza kuchapwa na mkewe. Kwa kawaida wanaume wanaamini kuwa wao ndiwo wenye mamlaka na uwezo wa kuwatawala wanawake katika ndoa. Kwao, mwanamke ni kitu kisichokuwa na nguvu wala uwezo na sharti kidhibitiwe na kukanyagiwa chini. Kwa kawaida hali ingekuwa tafauti iwapo ni mwanamume angeonekana akimcharaza mkewe. Wanajamii aghalabu hawatarajii mwanamke kumtawala mume katika ndoa. Mwanamume akimtesa na kumdhulumu mkewe kwa kumpiga katika ndoa, jamii inakubali hali hii kwa misingi kwamba sharti mwanamke atiwe adhabu ili anyooke kimaadili. Lakini mwanamume



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

aliyepotoka kimaadili akinyoroshwa na mkewe kwa kucharazwa, jamii inalalamika kwani mila na desturi zinazomkuza mwanamume kama hejemoni katika ndoa zinavunjwa.

Hejemonia katika ndoa pia ni suala ambalo limemulikwa katika *Msururu wa Usaliti.* Kwa mfano, Magu anamhadaa mkewe Naito kwa kutumia matendo mazuri ya kuonyesha uwajibikaji wa muda mfupi. Kwa kutambua kuwa tabia yake ya ulevi wa kupindukia na kutowajibika pale nyumbani ni sababu ya mkewe kumpuuza na kutomhusisha katika mipango yoyote muhimu pale nyumbani, Magu anaibuka na njama ya kumwonesha mkewe kuwa bado anamtawala. Magu anaamka asubuhi kukata majani ya kumlisha ng'ombe wakati wa kukama. Anayatia majani hayo kwenye hori na kuyakatakata na kisha kumwachilia ndama, kuandaa ng'ombe tayari kwa kukamuliwa. Ili kumfurahisha mkewe zaidi, Magu anapasua gogo la mti ili kupata kuni. Siku hii hata chamcha anakula nyumbani pamoja na mkewe. Ikumbukwe kwamba tukio hili ni kioja, hasa kwa Naito mkewe ambaye kwa miaka mingi hajamwona mumewe akifanya hivyo.

Katika *Msururu wa Usaliti* Magu anajitia kufanya kazi kwa nia ya kutumia fursa hii kama chambo cha kumnasa na kumshawishi mkewe. Mkewe alikuwa amekula yamini kumpuuza mumewe katika maandalizi ya makaribisho ya wageni. Matokeo ya hadaa hizi yakawa Naito kufungua moyo na kumtambua Magu kama mumewe. Akasahau uwovu wa Magu, akakumbuka uzuri wa mumewe. Magu anafaulu kumtawala tena mkewe kama mume wa boma (uk 191-192). Mwanamume huyu anatumia ujanja kupata anachotaka kutoka kwa mkewe. Wanaume wanakuza hejemonia katika ndoa kwa hadaa za kufanya kazi ambazo kwa kawaida hawazifanyi pale nyumbani. Wanaume wanaonesha mamlaka juu ya wake zao kwa kuwachezea akili. Matendo ya Magu yanamsawiri mwanamume kama hejemoni anayejua kumtuliza mkewe hususan katika hali ambayo mke hafai kukubali tabia ya mumewe. Kwa njia hii, wanaume wanafaulu kukuza na kuendeleza hejemonia katika asasi ya ndoa. Huu ni ujanja ambao wanaume wanatumia ili kutawala fikira, hisia na mawazo ya wanawake ili kwamba wapate wanachotaka hata kama wangenyimwa. Wanawake wanaoruhusu kuchezewa akili na waume zao wanachangia pakubwa kuwepo kwa hejemonia katika ndoa.

Hejemonia ya kijamii katika ndoa pia imeangaziwa katika *Msimu wa Vipepeo*. Kauli anazotumia Mkurutu anapozungumza na mkewe Julia, zinalenga kumshawishi amwamini. Kila wakati, waziri Mkurutu anamwambia mkewe: "Sio vyema kumsiriba binti mdogo kama huyu maadili yasiyofaa, unajua tunaishi katika ulimwengu usiojua amali zifaazo ni zipi," (uk 2). Kwa semi hizi, Julia anamwona Mkurutu kuwa mtu bora zaidi ambaye angekuja maishani mwake kabla ya kukutana na mumewe wa kwanza; Bw. Kanda. Utajiri wa waziri Mkurutu unamwaminisha Julia kuwa huyu ndiye mume bora zaidi ulimwenguni kote. Inasemekana Mkurutu anamiliki vifaa vya kisasa kama vile kitanda cha samadari, televisheni ya Sony Triniton ya inchi 34, mashini ya DVD, piano, makabati makubwa ya nguo, bafu la kisasa lenye bomba na legeni la kuogelea na godoro la maji. Vyote hivi na vingine vingi vinamridhisha na kumwaminisha Julia (msichana wa watu aliyezaliwa na kulelewa katika mazingira ya uchochole) kuwa Mkurutu alikuwa mume tosha bali sio gumegume.

Kama inavyodhihirika katika *Msimu wa Vipepeo* kupitia ndoa kati ya Waziri Mkurutu na Julia, hejemoni katika ndoa anaibuka na mawazo pevu anayoyawasilisha kwa mtawaliwa kwa maneno matamu ya kumtoa nyoka pangoni. Wanaume katika muktadha huu wanawapumbaza wake zao kwa maneno matamu ilmradi mamlaka yao yakubalike kwa hiari. Baadhi ya wanawake



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

katika ndoa wanakubali mamlaka ya waume zao kwa sababu ya tamaa ya kupata utajiri wa haraka. Wanawake wasio na uwezo wa kiuchumi katika ndoa wanaishia kuwategemea waume zao. Wanaume nao kwa kugundua udhaifu huu wanatumia mizungu ya ndoa kuibuka mahejemoni wanaowatawala wake zao kwa hali na mali. Wanawake wanaishia kuridhia chochote na lolote wanaloambiwa na waume zao ili wasipoteze manufaa wanayopata katika ndoa. Hali hii inakuwa tofauti kwa wanawake walio na uwezo wa kujitegemea kiuchumi kama tunavyoona katika ndoa baina ya Katumbi (mwalimu) na Munene (mfanyabiashara na mwanasiasa). Wanawake wenye uwezo wa kujitegemea wanapambana na wanaume wanaokuza na kuendeleza hejemonia katika jamii.

Miranda katika *Msimu wa Vipepeo* anasimulia kisa ambacho mwanamume mmoja wa kwao aliibuka kuwa hejemoni wa kupigiwa mfano katika jamii. Mke wa mwanamume huyo hakuwa na ajira yoyote na kwa hivyo akalazimika kukaa nyumbani huku akijishughulisha na kazi ndogo ndogo za pale nyumbani. Mumewe kwa kudhania kuwa mkewe ni kipepeo asiyetulia nyumbani, akaamua kuacha kazi mjini Kitambaasie na kurudi kijijini akae karibu na mkewe ili amchunge. Mwanamume huyu akakusudia kumtawala na kumwelekeza mkewe kwa kila kitu. Miranda akirejelea kisa hicho anaeleza:

> "Mama hata kuchimba viazi vitamu na mihogo lazima aelekezwe… chimba hapo…. Pale usiguse; akipika kuku wakati wa kula mwanamume anauliza, Ehh, kiga kile kingine kiko wapi? Mbona firigisi sioni? Mabawa amekula nani? Mbona supu imepungua… akawa anamkamata nzi na kutumbukiza kwenye karatasi ya kuhifadhi sukari, jioni akirudi anafungua karatasi yake kuangalia kama nzi wake, mtumwa ambaye ni mtego yupo, kama hayupo sukari yake imechotwa" (uk 169-170).

Baadhi ya wanaume katika ndoa ni kama mabepari na mabwanyenye wanaowadhibiti na kuwaelekeza wanafanyakazi kwa kila kitu. Wengine ni madikteta wanaowalazimisha wake zao kufanya wanavyotaka bila kuuliza chochote. Hawa ndiwo wanaoenda hatua ya kuwachunguza na kuwasimamia wake zao wanapofanya kazi yoyote. Wanaume kama hawa wanaamini kwamba hakuna kazi yoyote nzuri ambayo mwanamke anaweza kufanya ila kwa kusimamiwa na kuelekezwa kama mtoto anayezoeshwa kutambaa. Kwao, mwanamke ni mtoto tu hata kama ameolewa. Hejemonia inayokuzwa na wanaume katika ndoa inafaulu kwa sababu wanawake wanakubali hali hii. Wanawake wanaokubaliana na yote wanayoambiwa na waume zao kimsingi wanasaidia kukua na kudumu kwa hejemonia katika ndoa.

**Dini**

Hejemonia pia imejitokeza katika dini. Viongozi wa dini wana ushawishi mkubwa juu ya waumini na wafuasi wao. Viongozi hawa wanatumia nafasi yao kuwashawishi waumini wao kufanya watakalo. Mwandishi wa *Msururu wa Usaliti* anasema: "Wananchi… waliwasikiliza mapasta, wachungaji, mapadri na maaskofu wao… Mbunge au diwani aliyealika vita na makanisa alikuwa anajitia kitanzi kisiasa" (uk 3). Kwa sababu viongozi wa dini wana ushawishi mkubwa juu ya waumini wao, wanatumia uwezo wao kuwashawishi waumini waunge mkono kiongozi fulani wa kisiasa. Hivyo, viongozi wa dini wanatumia mizungu ya imani ya dini yao kuwatawala wafuasi na waumini wao. Kwa njia hii waumini wanaishia kufanya chochote wanachoambiwa na viongozi wao pasipo kuuliza maswali. Hali hii inadhihirisha namna viongozi wa madhehebu anuwai wanadumisha hejemonia katika dini zao.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Vilevile viongozi wa dini wanakuza na kudumisha hejemonia katika jamii kwa ushirikiano na viongozi wa kisiasa mintarafu *Msururu wa Usaliti.* Mapasta, maaskofu na makuhani wanaungana na viongozi wa kisiasa katika jamii kushawishi raia kuunga mkono mfumo fulani wa uongozi. Wanasiasa kama vile Mheshimiwa Mbogo wanahudhuria ibada ya kila Jumapili ili kuwashawishi waumini kuwa wao ni viongozi waadilifu na kwamba wako tayari kupambana na uwovu kwa mujibu wa mafundisho wanayopokea kanisani. Kwa njia hiyo, pamoja na kutoa sadaka kubwa kubwa na michango mingine mingi kama inavyoitishwa na viongozi wa dini, wanaungwa mkono na waumini wengi. Wafuasi wa madhehebu anuwai wanawasikiliza manabii, mapasata, wachungaji, mapadri na maaskofu wao. Kiongozi anayeonekana kukiri na kufuata imani ya dini fulani anapata uungwaji mkono kutoka kwa waumini wenzake wa dini husika. Ukweli kwamba wanasiasa wanahudhuria ibada katika makanisa mbalimbali na bado wanaendeleza uwovu kupitia uongozi wa kihejemonia ni kinaya na dhihaka kwa dini inayofaa kufunza maadili.

**Utamaduni**

Utamaduni ni asasi ya kijamii ambamo hejemonia inakuzwa na kudumishwa. Tamaduni nyingi katika riwaya teule zinamsawiri mwanamume akiwa hejemoni katika jamii. Katika *Msururu wa Usaliti,* uchumba kati ya Dkt. Makau na mwanasheria Nafula unavunjika kutokana na ubabedume wa Makau. Kwa kuamini utamaduni wa jamii yake, Dkt. Makau anataka kumtawala mchumba wake. Makau ni zao la utamaduni unaomfunza na kumwaminisha mwanamume kuwa ndiye mwamuzi, kiongozi na mtu muhimu katika jamii. Kulingana na mkabala huu wa mawazo ya kitamaduni, mwanamke sharti akubaliane na mwanamume. Mwanamke asiyekubaliana na yale mwanamume anasema anakosa heshima na kwa misingi hiyo mwanamke kama huyo hafai kuolewa. Wanaume wanatumia mila na desturi potovu kuwatawala wanawake. Baadhi ya wanawake wanashawishika na kukubaliana na matakwa ya jamii kwa misingi ya mila na desturi husika.

Kwa kuzingatia utamaduni, wanaume wanaendeleza hejemonia kwa kuwa wao pekee ndiwo wamiliki wa mashamba na mali. Wanaume kama vile Munene na babake ambaye alikuwa chifu wakati wa ukoloni ndiwo wamiliki wa mashamba na biashara kubwa kubwa katika *Dharau ya Ini*. Mheshimiwa Mbogo, Mzee Igweta na Kipanga katika *Msururu wa Usaliti* pia ni wamiliki wa mashamba. Katika *Msimu wa Vipepeo* wanaume kama vile Waziri Mkurutu, Fabio Mkalla na wawekezaji kama vile Gatusso Berlisconi ni mabepari wakubwa. Kadhalika, wanaume kama vile Wapukorengonyi na Baikungi ndiwo wamiliki wa mashamba makubwa, wakulima tambulika na wafugaji hodari katika jimbo la Miwambo mintarafu *Majilio ya Mkombozi.* Kwa upande mwingine, hamna hata mwanamke mmoja anayemiliki mashamba wala mtaji wa biashara au hata kuwa katika wadhifa wa uongozi katika jamii zinazosawiriwa riwayani. Utamaduni unatumika kuwanyenyekeza wanawake na kuwaweka chini ya utawala wa wanaume. Mila na desturi zinazozohusiana na umilikaji wa mali zinamridhisha mwanamke kuamini kwamba ardhi na nyenzo zote za uzalishaji mali ni milki ya mwanamume. Hali hii ni msingi wa kuwepo hejemonia katika asasi ya utamaduni wa jamii. Utamaduni unawafinyanga wanaume kuwa mabepari na mabwanyenye wanaomiliki mashamba na chochote kitokacho shambani. Hivyo, mwanamume anakuza na kuendeleza hejemonia kwa kumwaminisha mwanamke na jamii kwa jumla kuwa mali yote ni milki yake.

Katika *Majilio ya Mkombozi,* Shahiruzode mke wa Baikungi anapinga utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya uongozi na kushiriki katika utatuzi wa mizozo anuwai katika jamii. Anasema: "Huo ni mwelekeo wa kizamani, mambo yamebadilika. Sauti ya mwanamke ni



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

lazima isikike kwani jambo lililotokea haliwahusu wanaume pekee bali familia yote" (uk 102-103). Mwanamke huyu anakosoa na kupinga utamaduni unaotetea uhafidhina katika jamii. Anataka watu wote wahusishwe katika michakato ya kusuluhisha matatizo yanayoikumba jamii kinyume na utamaduni unaowapa wanaume kipaumbele. Kimsingi, anapinga hejemonia inayokuzwa kwa misingi ya utamaduni wa jamii. Wanawake sharti waelewe kuwa upole ukizidi unaendeleza uhalifu. Ufahamu wa namna hii unawasaidia kukabiliana na hejemonia ya kijamii inayokuzwa na kudumishwa katika utamaduni unaowapa wanaume mamlaka makubwa.

Kwingineko, baadhi ya wanawake kama vile Julia katika *Msimu wa Vipepeo* na Kasina katika *Dharau ya Ini* wanaishia kuridhia na kuidhinisha utawala wa mwanamume kwa madai kwamba wanatimiza mila na desturi za jamii. Hali hii imemfanya mwanamke kuwa mtegemezi wa mwanamume kwa mambo mengi katika jamii. Utamaduni wa jamii unamfanya mwanamume kuwa hejemoni ambaye sharti wanawake wakubaliene naye iwapo wanataka manufaa yoyote. Mwanamume, kwa hivyo anaendeleza utawala wa kihejemonia katika jamii kwa kupigwa jeki na mwanamke anayeridhia matakwa ya utamaduni.

Hejemonia na utamaduni ni suala ambalo limeshughulikiwa na mwandishi wa *Majilio ya Mkombozi.* Katika jimbo la Miwambo kunafanyika mashindano ya kitamaduni ya kupiganisha mafahali ambapo mshindi katika mchezo huo anatuzwa mabeberu watatu. Pia, anapata umaarufu na sifa za mfugaji bora na hodari. Utamaduni wa watu wa Miwambo unafuata sheria ambazo sharti zifuatwe kwa utaratibu. Kwanza, washirika wawe watoto wa kiume wa kwanza wa familia husika. Pili, sheria inamruhusu mpwa kumleta fahali wa mjomba wake. Ingawaje mchezo huo wa kitamaduni umechukua sura ya shughuli za kijamii, suala la hejemonia limeangaziwa kwa uzito. Ukweli kwamba utamaduni unahitaji watoto wavulana wawe washiriki huku wasichana wakikosa wajibu wowote katika mchezo ni ubaguzi wa kijinsia wenye misingi yake katika ubabedume na hejemonia. Utamaduni kama huu unakuza na kuendeleza hejemonia kwa kuwaandaa vijana wa kiume kuchukua majukumu ya utawala juu ya wenzao wa kike katika jamii. Vijana wavulana wanapokua na kisha kuingia katika utu uzima wanaishia kuwa mahejemoni katika jamii kwani utamaduni wa jamii uliwazoesha mapema. Kwa hivyo, utamaduni unakuza hejemonia kwa kumwaaminisha mwanamke kwamba hapana haja ya yeye kushiriki katika maswala ya uongozi wa kijamii.

Hejemonia katika utamaduni inajitokeza katika riwaya ya *Dharau ya Ini*. Kwa mfano, msimulizi anatujuza kuwa, walipokuwa wadogo walishikwa sikio na kubinywa kila wakati wakifunzwa kuwa; "Msichana hakai hivi. Msichana hacheki ovyo. Utamaduni. Desturi. Mila. Babu… Mwanamume," (uk 4). Watoto wavulna nao waliachiliwa huru. Hii inamaanisha kwamba kwa mujibu wa utamaduni, mwanamke anafaa kuwa makini siku zote, awe mtiifu kwa sheria ambazo zimewekwa. Wanawake nao wanasadiki na kufuata desturi za jamii yao; desturi na mila zinazowekwa kukuza hejemonia. Mila na desturi kama hizi zinawatetea wanaume katika jamii na kuwafinyanga kuwa mahejemoni. Hivyo, wavulana wanakua wakijua kwamba wasichana ni viumbe dhaifu ambao sharti waelekezwe kwa kila kitu. Utamaduni huu unawafanya wanaume wawatawale wanawake kwa mambo mengi. Matokeo ya hali hii ni wanaume kuwa mahejemoni wanaowadunisha na kuwadhalilisha wanawake kwa misingi ya kufuata utamaduni. Kwa kuamini utamaduni, wanawake wanawaacha wanaume watawale na hivyo basi hejemonia inanawiri.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Hejemonia pia inajitokeza katika utamaduni unaohusiana na mwanamke kupata mtoto katika ndoa mintarafu *Dharau ya Ini na Msimu wa Vipepeo*. Katika *Dharau ya Ini* Munene anawapiga wake zake Kasina na Katumbi kwa kutomzalia mtoto wa kiume. Katika *Msimu wa Vipepeo*, mwanamke asipomzalia mwanamume mtoto, mwanamume anatumia hicho kama kisingizio cha kumwendea mkewe kinyume katika ndoa. Mwanamume anamchukulia mwanamke kama mtambo wa kuzaa. Julia, akionyesha kutoridhishwa na hali hii anasema: "Ingekuwa watoto wanatagwa ningetaga nikamwachia yai lenyewe alilalie na kulitotoa!" (uk 95). Utamaduni wa namna hii unaoaminisha jamii nzima kwamba sharti mwanamke awe na uwezo wa kuzaa ndiposa akubalike katika jamii unaenda kinyume na ukweli wa sayansi ya kibiolojia. Mwanamume au mwanamke katika ndoa kwa mujibu wa sayansi, yeyote kati yao anaweza kukosa uwezo wa kupata mtoto kwa sababu za kiafya. Imani kuwa watu wazima katika ndoa wasio na uwezo wa kupata watoto ni watoto, ni mawazoganda yanayoendelezwa na hejemonia katika utamaduni ili kuwanyima wanawake usemi katika jamii husika. Hivyo, hejemonia inajitokeza katika utamaduni pale ambapo wanaume wanawatawala wanawake kwa misingi kwamba wanawake wasioweza kuzaa wanaenda kinyume na matarajio ya utamaduni.

Hejemonia inajitokeza pia katika utamaduni ambao unawanyima wanawake uhuru wa kuvaa aina fulani ya mavazi na kula aina fulani ya vyakula kama inavyodhihirika katika *Dharau ya Ini* na *Msimu wa Vipepeo*. Katika *Dharau ya Ini* Munene anamkemea Lila kwa kuvaa suruali ndefu kwani ni kinyume na utamaduni. Katika *Msimu wa Vipepeo* utamaduni haumruhusu mwanamke kula viga vya kuku, kichwa cha ng'ombe au mbuzi, ini pamoja na mapafu. Hali hii inaonyesha mamlaka na utawala wa mwanamume juu ya mwanamke katika utamaduni wa jamii. Utamaduni unamfinyanga mwanamume na kumfanya kuwa hejemoni wa kumtawala mkewe. Wanaume wanakuza na kudumisha hejemonia ya kijamii katika utamaduni kama huu. Wanawake wanaosadiki na kukubali hali hii wanafanya hivyo kwa imani kuwa hawataki kuwa watumwa wanaosemekana kuvunja mila na desturi za jamii. Hejemonia inadumishwa katika utamaduni wa jamii kwa idhini ya wanajamii.

Utamaduni unaonekana kusheheni hejemonia pale ambapo wanaume hawalaumiwi kwa kuwa na watoto nje ya ndoa badala yake wanawake wanabebeshwa lawama hiyo. Kwa mfano, kisa cha Miranda kuzaliwa nje ya ndoa katika *Msimu wa Vipepeo* na vile vile kisa cha Mheshimiwa Mbogo kumbaka mjakazi katika *Msururu wa Usaliti.* Kadhalika, kijana Yunga Mwamba katika *Dharau ya Ini* alizaliwa na kutokana na Munene kumbaka Kasina ambaye ni somo wa mke wake. Utamaduni unamlaumu mwanamke kwa kuzaa nje ya ndoa kana kwamba kitendo cha kujamiana kinafanyika kati ya mwanamke na mwanamke mwenzake. Mwanamume anachangia kuwepo kwa watoto wanaozaliwa nje ya ndoa kwa kujihusisha kimapenzi na wanawake huku akijua kuwa hayuko tayari kuwaoa. Hivyo, inasikitisha kutambua kwamba utamaduni unamkashifu mwanamke anayezaa nje ya ndoa huku mwanamume anayempachika mimba akiachiliwa huru. Hejemonia ya kijamii inadhihirika katika mazingira haya ambapo wanaume wanatumia mizungu ya utamaduni kuwatawala wanawake katika jamii.

Hejemonia ya kijamii kadhalika inadhihirika katika jamii anakotoka Rais Kamaliza Rungu-ya-Kioga katika *Msimu wa Vipepeo*. Matanu akimweleza Melissa kuhusu matokeo ya utafiti waliofanya kuhusu utamaduni wa jamii hiyo anasema hivi:

> "Watoto wanaanza kupewa ziwa la mama wakiwa wiki tatu baada ya kuzaliwa… kwa



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

> sababu dang'a katika jamii hiyo sio ya watoto…jamii inasema kuwa dang'a ni ya mwanamume sio mtoto mchanga… ni haki yao wanasema! ... wanasema hivyo ndivyo ulivyo utamaduni wao tangu zamani" (uk 192).

Utamaduni wa jamii hii unawasawiri wanaume kama wanyonyaji wa wanawake. Unyonyaji wenyewe unaishia kuwanyima watoto haki yao. Si ajabu basi kupata kwamba watoto katika jamii hiyo wanasumbuliwa na magonjwa ya kuendesha na maradhi mengi kama vile mafua kwa sababu ya kukosa kinga ya awali inayohusishwa na maziwa ya mama. Utamaduni unatumiwa kama msingi wa kuendelea kufyonza damu ya kiwiliwili cha jamii hadi pale jamii inashindwa kuhimili na kuanguka kwa kishindo. Jamii inafumbwa macho na kuruhusu hali hii. Kimsingi, jamii inafaa kupinga uwepo wa hali hii lakini inahadaiwa kukubali hali ilivyo. Hivyo ndivyo hejemonia inavyokua na kuendelea kutokana na kutojali kwa raia wanaothamini utamaduni wa jamii.

Katika *Msimu wa Vipepeo,* hejemonia vilevile inajitokeza kupitia utamaduni unaompa mwanamume mamlaka makubwa juu ya mkewe kiasi kwamba sharti mke atafute kibali kutoka kwa mumewe kabla hajapata huduma muhimu katika afisi za umma. Kwa mfano, Melissa anapoenda kutafuta pasipoti ya usafiri, anapigwa na butwaa anapoambiwa kwamba sharti apate kibali kutoka kwa mumewe. Afisa wa kutoa pasipoti anasisitiza hivi, "…lazima mumeo atoe kibali! Hivi ndivyo utamaduni unavyosisitiza na kama hujui, utamaduni ni kitovu cha uhai wa taifa hili" (uk 192). Pia mwanamke hawezi kuzuru hoteli yoyote ya kifahari bila ya kuambatana na mwanamume. Mathalani, katika hoteli ya *The Peacork*, wanawake hawaruhusiwi kuingia huko bila mwanamume. Mwandishi anasema:

> "Kuna siku moja mwanamke mmoja, Profesa mzima tena, kutoka chuo kikuu cha Kitambaasie alipoenda hoteli ya *The Peacork* akazuiliwa mlangoni!... walimwambia hawaruhusu wanawake wasioambatana na wanaume!" (uk 169).

Wanawake wanadhalilishwa na utamaduni unaowakweza wanaume. Jambo la kushangaza ni kwamba hakuna sheria ya kitamaduni inayomtaka mwanamume pia aandamane na mkewe kabla hajaruhusiwa kuingia hotelini au kupata huduma za umma. Mkondo huu wa mambo unadhihirisha hejemonia katika utamaduni wa jamii. Utamaduni wa jamii unampa mwanamume mamlaka makubwa juu ya mkewe. Mwanamke anafanyanywa kuwa kiumbe cha kudhibitiwa kwa tuhuma kwamba yawezekana amwendee mumewe kinyume katika ndoa. Mwanamume naye anaibuka kuwa hejemoni mkubwa kwa kuwachwa huru bila ya masharti sawia na yale anayowekewa mwanamke.

**Hitimisho**

Mintarafu utafiti huu, imebainika kwamba safu ya hejemonia ya kijamii inadhihirika katika asasi anuwai. Asasi hizi ambamo hejemonia imedhihirika ni kama vile taasisi za elimu, dini utamaduni, ndoa na malezi katika familia. Katika asasi zote, imewekwa bayana kuwa watu wenye mamlaka juu ya wenzao kama vile wazazi, wanaume, wanawake, viongozi wa dini na viongozi wengine katika jamii wanadhihirisha sifa za mahejemoni. Aghalabu watu hawa wanatumia vishawishi anuwai kudumisha hejemonia katika asasi hizo za kijamii. Muhimu ni kwamba, watawaliwa katika asasi zote za kijamii wanaidhinisha kuwepo kwa hejemonia wanaporidhia na kuidhinisha vishawishi vinavyotumiwa na watawala. Hata hivyo, baadhi ya watawaliwa kwa kugundua hila na hadaa katika vishawishi vya watawala wanaishia kukosoa na kupinga hejemonia katika jamii.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v2i1.130
ISSN: 2663-9289
Volume: 02 Issue: 01 | June-2020|
Received: 17.06.2020; Accepted 19.06.2020; Published on 30.06.2020 at www.editoncpublishing.org
Ogutu, H. O., et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**Mapendekezo**

Mapendekezo yetu hapa ni kuwa watafiti wa baadaye wanaweza kushughulikia mada zingine kama vile; mchango wa wanawake katika jamii yenye hejemonia na uchunguzi wa changamoto zinazowakumba viongozi wanaokuza hejemonia katika jamii.

**MAREJELEO YA KIMSINGI**

Mbatiah, M. (2016). *Majilio ya Mkombozi.* Nairobi. Moran (E. A) Publishers Limited.
Mbatiah, M. (2010). *Msururu wa Usaliti.* Nairobi. East African Educational Publishers Limited.
Wamitila K. W. (2007). *Dharau ya Ini.*Nairobi. Vide-Muwa Publishers Limited.
Wamitila K. W. (2006). *Msimu wa Vipepeo*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers Limited.

**MAREJELEO MENGINE**

Artz, L. & Murphy, B. O. (2000). *Cultural Hegemony in the United States*. California: Sage Publications.
Gramsci, A. (1995). *Further selections from the prison Notebooks.* Edited and translated by Derek Boothman. Minneapolis: University of Minnesota press.
Meysam, A. (2014). *Cultural Hegemony in Charles Dicken's A Tale of Two Cities.* International Journal of Literature and Arts. Vol 2, No 4. Uk 98-103. Published online July 20, 2014. Ilitembelewa 15/09/2018, 10:30. http://www.sciencepublishinggroup.com/j/ijla
Nella, P. (2017). *The Many Faces of Power:* The Portrayal of Hegemony in *Fight Club* by Chuck Palahniuk and *American Psycho* by Bret Easton Ellis. University of Tamperes Press.
Strinati, D. (1995). *An Introduction to the Theories of Popular Culture*. London. Routledge.
Wamitila K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publications Limited.



© 2020, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org